# Nation Printers and Publishers Limited



DT
448.2
.K46
N385
1996

Report and Accounts 1996 • Ripoti na Hesabu ya Pesa 1996

# Contents

# Yaliyomo


| | Page *Ukurasa* |
|---|---|
| Mission statement and annual highlights 1996 | 2 |
| *Wito wa kundi na matukio muhimu ya mwaka 1996* | *2* |
| Notice of Annual General Meeting | 3 |
| *Tangazo la Mkutano wa kila Mwaka* | *3* |
| Chairman's statement | 4 |
| *Ripoti ya mwenyekiti* | *9* |
| Board of directors | 14 |
| *Halmashauri ya wakurugenzi* | *15* |
| Directors' report | 16 |
| *Taarifa ya wakurugenzi* | *17* |
| Report of the auditors | 18 |
| *Taarifa ya wakaguzi wa hesabu* | *19* |
| Group profit and loss account | 20 |
| *Hesabu ya faida na hasara ya kundi* | *21* |
| Balance sheets | 22 |
| *Hesabu ya fedha* | *23* |
| Group cash flow statement | 24 |
| *Mapato na matumizi ya fedha ya k* | *25* |
| Notes to the accounts | 26 |
| *Maelezo juu ya hesabu* | *27* |
| Five year financial summary | 38 |
| *Taarifa fupi ya kifedha ya miaka mitano* | *38* |
| Proxy form | 39 |
| *Fomu ya uwakilishi* | *40* |



CMA – Ke Library

AR0250

CMA - LIBRARY

CMA - LIBRARY


***Front cover***

1. *The new printing press, Mombasa Road.*
2. *President Moi opens the new press in the presence of His Highness The Aga Khan.*
3. *The chairman makes his address.*
4. *A childrens' choir entertains the guests.*

***Picha za mbele***

1. *Kiwanda kipya cha uchapishaji katika Mombasa Road.*
2. *Rais Moi akifungua kiwanda hiki kipya akiwemo Mtukufu Aga Khan.*
3. *Mwenyekiti akitoa hotuba.*
4. *Kwaya ya watoto ikitumbuiza wageni.*

***Back cover***

1. *His Highness The Aga Khan presents long service awards.*
2. *The Nation Centre, Kimathi Street.*
3. *His Highness The Aga Khan studies the Nation Internet site.*

***Picha za nyuma***

1. *Mtukufu Aga Khan akikabidhi vyeti vya utumishi wa muda mrefu.*
2. *Nation Centre, Kimathi Street.*
3. *Mtukufu Aga Khan akichunguza jinsi kifaa cha Nation Internet kinavyofanya kazi.*

Nation Media group --- Periodicals
2 Media group --- Kenya -- Periodicals

DT
448.2
.K46
N385
1996.

# Mission Statement and Annual Highlights 1996

## Mission statement
To be the most successful media group in East Africa.

## Annual highlights 1996
Total revenue increased by 23% to Kshs. 1.9 billion.

New printing plant brought on stream on time and within budget.

Operating profit before interest improved by 21% to Kshs. 357.4 million.

The outstanding $33\frac{1}{3}$% of Nation Carriers Limited acquired from Akamba Public Road Services Limited.

The group's interest in Industrial Promotion Building Limited increased from 16.4% to 20%.

41.7% interest in Kenya Litho Limited sold for an extraordinary profit of Kshs. 48.0 million.

Profit attributable to shareholders increased by 6% to Kshs. 206.9 million.

Recommended dividend total of 55%, an increase of 22% over 1995.

Proposed one for two bonus share issue.

# Wito la Kundi na Matukio Muhimu 1996

2007/0250

## Wito la kundi
Kuwa kundi la kufaulu zaidi la habari katika Afrika Mashariki.

## Matukio muhimu ya 1996
Mapato kwa jumla yaliongezeka kwa asilimia 23% hadi Kshs. 1.9 bilioni.

Mitambo mipya ya uchapishaji yaletwa na kufunguliwa katika wakati na bajeti iliyokadiriwa.

Faida ya kibiashara kabla ya riba inaongezeka kwa asilimia 21% hadi Kshs. 357.4 milioni.

Hisa asilimia $33\frac{1}{3}$% ya Nation Carriers Limited zanunuliwa kutoka kwa Akamba Public Road Services Limited.

Hisa za kundi katika Industrial Promotion Building Limited zaongezeka kutoka asilimia 16.4% hadi asilimia 20%.

Hisa asilimia 41.7% katika Kenya Litho Limited ziliuzwa kwa faida ya ajabu ya Kshs. 48.0 milioni.

Faida kwa wenye hisa iliongezeka kwa asilimia 6% hadi Kshs. 206.9 milioni.

Mgawo uliopendekezwa wa faida wafikia jumla ya asilimia 55%, ongezeko la asilimia 22% juu ya 1995.

Toleo lililopendekezwa la hisa mbili za bakshishi kwa kila hisa moja inayohifadhiwa.

# Notice of Annual General Meeting

Notice is hereby given that the thirty fourth Annual General Meeting of the shareholders of Nation Printers and Publishers Limited will be held at the Hotel Inter-Continental, Nairobi, on Thursday, 12 June, 1997 at 3.00 p.m. for the following purposes:–

**Ordinary business**

1 To receive the accounts for the year ended 31st December, 1996 and the chairman's, directors' and auditors' reports thereon.

2 To confirm the payment of the interim dividend of 12.5% and to approve the payment of a final dividend of 42.5% on the ordinary share capital in respect of the year ended 31st December, 1996.

**Special business**

3 To resolve that it is desirable to capitalize the share premium account amounting to Kshs. 1,327,220 together with part of the revenue reserves of the company amounting to Kshs. 28,383,305 and that the same be applied in paying up in full at par 5,942,105 shares of Kshs. 5.00 each in the capital of the company, such shares to be allotted and distributed as fully paid up to the shareholders who are registered at the close of business on 30th May 1997 in the proportion of one such new share for every two existing shares held by such member respectively (fraction of a share to be disregarded) and further that such shares shall rank pari passu with the existing shares except that they shall not qualify for the payment of the final dividend for the year 1996 declared by this meeting and the directors are hereby authorised to give effect to this resolution.

**Ordinary business**

4 To authorise the directors to fix the remuneration of the auditors, Messrs Coopers & Lybrand.

5 To elect and re-elect the following directors:
In accordance with Article 96 of the Articles of Association, Mr. R. C. Henry being eligible, offers himself for re-election.

In accordance with Article 110 of the Articles of Association, Mr. H. H. O. Awori, Mr. A. Poonawala and Mr. W. Robinson retire by rotation and, being eligible, offer themselves for re-election.

6 To transact any other competent business.

By order of the Board
S. G. Ogutha
Secretary 10th April, 1997

Note:
A member entitled to attend and vote may appoint a proxy to attend and vote for him on his behalf. Such proxy need not be a member of the company. To be valid, proxy forms must be deposited at the company not less than 48 hours before the appointed time of the meeting.

# Tangazo la Mkutano Mkuu wa kila Mwaka

Notisi inatolewa hapa kwamba Mkutano mkuu wa kila mwaka wa thelathini na nne wa wanachama wa Nation Printers and Publishers Limited utafanywa hoteli ya Inter-Continental, Nairobi, Alhamisi, Juni 12, 1997, saa tisa alasiri, kwa shughuli zifuatazo:–

**Shughuli za kawaida**

1 Kupokea na kujadili hesabu za mwaka uliomalizika Desemba 31, 1996 na ripoti za mwenyekiti, wakurugenzi na wakaguzi wa hesabu.

2 Kuthibitisha ulipaji wa mgawo wa muda wa faida wa asilimia 12.5 na kuidhinisha malipo ya mwisho ya mgawo wa faida wa asilimia 42.5 kuhusu mtaji wa hisa za kawaida kuhusiana na mwaka uliomalizika Desemba 31, 1996.

**Shughuli maalum**

3 Kuamua kwamba inafaa kutumia kiasi cha Kshs. 1,327,220 za akaunti kuu ya hisa pamoja na akiba ya mapato ya kampuni cha jumla ya Kshs. 28,383,305 na pesa hizo pia zitumiwe kulipa hisa 5,942,015 za Kshs. 5.00 kila moja katika rasilmali ya kampuni, na hisa kama hizo zitolewe na kugawanywa kama zilizolipwa na wenye hisa ambao walikuwa wameandikishwa wakati wa kufunga biashara mnamo Mei 30, 1997 kulingana na ulipaji na hisa moja kama hiyo kwa kila hisa mbili zilizoko alizo nazo mwanachama kama huyo (kifungu cha hisa kutotiwa maanani) na zaidi ni kwamba hisa kama hizo zitaenda sambamba na zile zilizoko ila tu kwamba hazitaweza kulipwa wakati wa mgawo wa mwisho wa mwaka 1996 unapotangazwa na mkutano huu nao wakurugenzi wanaidhinishwa kukubaliana na pendekezo hili.

**Shughuli za kawaida**

4 Kutoa idhini kwa wakurugenzi waamue marupurupu ya wakaguzi wa hesabu, Messrs Coopers & Lybrand.

5 Kuwachagua na kuchagua tena wakurugenzi wafuatao:
Kulingana na kifungu cha 96 cha Kanuni za Kampuni, Bw. R. C. Henry, kwa sababu anaweza kugombea uchaguzi, anajitolea kusimama kuchaguliwa tena kama mkurugenzi.

Kulingana na kifungu cha 110 cha Kanuni za Kampuni, Bw. H. O. Awori, Bw. A. Poonawala na Bw. W. Robinson wanastaafu kwa zamu na lakini kwa sababu wanaweza kugombea uchaguzi, wanaweza kusimama kuchaguliwa tena.

6 Kujadili mambo mengine yo yote yatakayostahili.

Kwa amri ya Halmashauri
S. G. Ogutha
Katibu Aprili 10, 1997

Muhimu:–
Mwanachama mwenye haki ya kuhudhuria na kupiga kura anaweza kumteua Mwakilishi (proxy) kuhudhuria mkutano na kupiga kura kwa niaba yake. Mwakilishi huyo si lazima awe mwanachama wa kampuni. Ili zitumike kihalali, Fomu za uwakilishi (proxy forms) zinapaswa kupelekwa katika afisi ilikoandikishwa kampuni masaa 48 kabla ya muda uliotengwa wa mkutano.

# Chairman's Statement



**Group performance**

The last year was one of significant progress for your group. The Kenyan economy remained buoyant throughout the first half of the year. However, this was not sustained in the second half during which economic growth was substantially less than the 5% recorded in the first six months.

Last year I referred in my report to progress following the Board's decision to replace the group's ageing printing plant. Work on the new press at our Mombasa Road site started in December 1995 and within twelve months the plant was in full production. Commissioning the German firm Koening and Bauer-Albert AG, we have installed presses capable of running at 60,000 copies per hour.

Not only was this major project achieved within the very tight timetable established, it was also achieved within the original budget of Kshs. 750 million. We now have a world class printing facility which is among the most advanced anywhere in Africa. Our investment, one of the largest by any private sector company in Kenya, enables us significantly to enhance the quality, size and colour content of all our publications.

The inauguration of the new Nation press took place in March in the presence of His Excellency the President of Kenya; and the principal shareholder, His Highness the Aga Khan together with many other distinguished guests. The success of the occasion was a testimony to the hard work and determination of all those involved.

The strong cash flow generated by the group in recent years meant that more than half the cost of the new press was internally generated with the balance borrowed by means of medium term bank loans. Despite the consequent sharp increase in loan interest payable, I am delighted to report that the group has again achieved record results.

Overall group revenue improved by 23% to Kshs. 1,895.7 million (Kshs. 1,538.0 million in 1995). Again, Nation Newspapers Limited was the main engine behind the group's performance with operating profit moving ahead by 25%. Group operating profit at Kshs. 357.4 million (Kshs. 294.7 million) was 21% ahead of 1995. However, group profit before taxation and extraordinary items at Kshs. 262.1 million (Kshs. 296.9 million) was Kshs. 34.8 million lower than last year, due to the sharp increase in interest paid as a result of the investment in the new press. Despite the additional interest costs of Kshs. 79 million, profit attributable to shareholders, after extraordinary items, at Kshs. 206.6 million (Kshs. 195. 1 million) was 6% ahead of the previous year.






*A historic meeting of President Clinton with Middle East leaders in Washington*

*Rais Clinton na viongozi Wakuu wa Mashariki ya Kati*

**Nation Newspapers Limited**

The group's principal subsidiary company again achieved record turnover and profitability in 1996. The cover prices of the *Daily Nation* and *Sunday Nation* were increased by Kshs 5 in March 1996. This was the first increase for two years and was actually below the rate of inflation for that period. The normal initial fall in sales of both titles following the increase was small and had been fully recovered by the year end. Both of the company's Swahili papers *Taifa*



*Kenya's Harambee Stars draw with Nigeria's Super Eagles in World Cup qualifiers*

*Harambee Stars ya Kenya ilienda sare 1-1 na Super Eagles ya Nigeria kwenye mechi ya maondoano ya Kombe la Dunia*

*Leo* and *Taifa Jumapili* witnessed useful gains in circulation during the year. At the same time, the company's regional weekly paper The *EastAfrican*, started in 1994, saw a strong increase in circulation as the paper firmly established itself throughout Kenya, Uganda and Tanzania as the required quality business newspaper for East Africa. Not only did the *EastAfrican* achieve its editorial circulation and advertising objectives, it also moved into profit during the year. This was a major achievement for such an ambitious concept. The newspaper has continued to receive wide acclaim not only throughout the region but even further afield.




For all our publications advertising remained strong throughout the year with excellent growth in revenue and volume despite significant ratecard increases early in the year. As a result the *Nations* and *Taifas* again saw useful increases in their advertising market share. The results are a tribute to both the readers' and advertisers' perceptions of the high quality of the company's English and Swahili publications.

The increased circulation and advertising revenues were the main contributors to the company's improved turnover of Kshs. 1,877.7 million, an increase of Kshs. 384.7 million (26%) over 1995.

Newsprint prices which had increased sharply in 1995, were virtually static during the first half of the year before falling steadily in the second half and, as a result, for the year as a whole, the increase was held to Kshs. 78.0 million (16% above 1995). However, other costs increased by more than 30% as a result of the company's commitment to the quality of its publications and maintaining remuneration levels commensurate with comparable Kenyan companies.

The overall level of increase in costs also reflected historic high levels of inflation. However, with inflation currently lower than for a very long time, future increases in costs are expected to be substantially lower than in 1996 as a result of vigorous cost controls and, to date, only modest increases in raw material costs.

A major and continuing goal again in the past year has been quality improvement. Editorial workshops with specific aims related to quality and policy objectives have instilled an increased level of awareness in our staff.

With the new press now in operation, the opportunity has been taken to review the company's colour policy. The Board has decided to pursue a careful programme of improved colour quality and steadily increased usage throughout our publications all linked to further significant pre-press investment. The majority of our pictures are now taken using colour film and appropriate use of colour will be gradually reflected over the coming months.

A further significant development during the year was the transition from cut-and-paste page make-up to electronic full page make-up. This was facilitated by new investment in the editorial and advertising departments where staff have now taken over the tasks traditionally done by pre-press staff. This has enabled us to derive maximum gains in terms of cleaner products and improved deadlines.

The *EastAfrican* entered its second year enjoying steadily growing circulation and





*The Lydia Achieng' Abura group performs at a music extravaganza in Nairobi*

*Waimbaji wa kundi la Lydia Achieng' Abura wakitumbuiza kwenye tafrija ya muziki mjini Nairobi*

advertising and with its position now firmly secured in the regional newspaper market. Circulation rose rapidly and by its peak in the last quarter of 1996 had increased by almost 70% since the start of the year. The *EastAfrican's* core readership, consists of the business and professional communities in the three countries and much of the advertising is business-to-business, further evidence of how the publication is perceived in the market as an effective medium for reaching investors, traders, professionals and decision makers across East Africa and elsewhere. As further evidence of this expansion additional distributors have been appointed in Harare and Johannesburg.

In recent months the company has initiated a number of developments to consolidate its presence on the World-Wide Web, with the aim of being the leading source on the Internet for African news and information, which fits well with our aim of being the leading media group in East Africa. The *Nation* Internet edition has also been expanded to include the Nairobi stock market as well as foreign stock exchange reports and is regularly consulted in countries as dispersed as Norway and the United States.

### Nation Marketing and Publishing Limited

Last year I reported that, as a result of the poor performance of Nation Marketing and Publishing Limited, its activities were being reviewed. As a result of this review your Board decided to cease the company's activities in certain areas. Nevertheless, as the economy and tourism improve, prospects for related publications should reappear. The company will therefore be looking at the possibility of reviving at least some of the titles through collaborative agreements with the aim of enhancing profitability in the future.

### Nation Carriers Limited

At the end of 1996, which was the second year that Nation Carriers Limited had been under the group's direct management, Nation Printers and Publishers acquired the outstanding 33 $^1/_3$% from Akamba Public Road Services Limited, making Nation Carriers Limited a 100% group subsidiary.

During the year the company performed outstandingly well in coping with the demands on the vehicle fleet from increased circulation and pagination. Despite the appalling and deteriorating road conditions throughout most of the country, deadlines were generally met and there was a reduction in accidents and breakdowns. However, this was again achieved at a very high cost in terms of vehicle renewal and maintenance, with the average life of the majority of the company's vehicles now less than three years.

We are confident that the encouraging trends of this subsidiary over the past two years will not only be maintained but improved on. The Board has approved plans to relocate the company in 1997 adjacent to Nation Newspapers new printing plant at the group's Mombasa Road site to ensure increased future efficiencies.

### Industrial Promotion Building Limited

As previously reported, when Industrial Promotion Building Limited (IPB) acquired Diamond Trust Properties Kenya in 1994, the Nation groups's interest in IPB fell from the 20% it had held since 1988 to 16.4%. At the end of 1996, IPB had a rights issue and, with the new press investment complete, Nation Printers and Publishers took the opportunity not only to take up its rights, but to acquire the additional shares necessary to increase its holding to 20% and thereby restore IPB to associated company status.

IPB owns the Nation Centre and the prestigious Nairobi city



*Chechens celebrate the fifth anniversary of the "declaration of Chechen Independence" from Rusia*

*Wakazi wa Chechen wakisherekea mwaka wa tano wa "kufangaza Uhuru wa Chechen" kutoka kwa Warusi*

centre IPS building amongst other properties. The company which has recently acquired a prime development site in Mombasa, has seen its trading performance continue to improve.

**Kenya Litho Limited**

Last year I reported that the funding requirements for the re-equipment of Kenya Litho Limited would make increasing demands on the company's cash resources during the coming years. In the light of this and the very significant demands faced by Nation Newspapers Limited for the new printing plant, your Board decided to sell its 41.7% holding in order to concentrate resources on the group's principal activities. I am pleased to report an extraordinary gain on disposal of Kshs. 48.0 million.



*President Mandela with President Moi ahead of the Great Lakes Crisis Region Conference*

*Rais Mandela na Rais Moi walipohudhuria mkutano wa Eneo la Mataifa ya Africa ya Kati*

**Broadcasting**

In past years the Chairman's report has referred to the group's aspirations to diversify into both radio and television broadcasting throughout the East African region.

Much work has been done by your management, more particularly so in the past year, to identify and develop the necessary strategy. It is again disappointing to have to report that to date no visible progress has been made in achieving licences in Kenya, although renewed applications have been made for both radio and television licences.

It is now six years since, in line with the government's commitment to freeing the airwaves, the Nation group applied for broadcast licences. It would be dishonest to pretend that your Board is not disappointed by the lack of a positive response to date, particularly as the group has continued to demonstrate a level of professionalism as a media organisation which we believe is unmatched by any of our competitors throughout the region.

Throughout the world, media organisations such as ours increasingly view themselves as being involved in the broad communications industry and have thus been participating actively in the explosion in both terrestrial and satellite broadcasting as well as the more recent development of the Internet.

In this same connection a recent event which can be expected to have far reaching implications for the media as a whole has been the publication of the *National Communications Bill* in the context of the restructuring of the Kenya Posts and Telecommunications Corporation. The bill, drafted for the purpose of among other things determining an appropriate framework for broadcast frequency allocations, appears also to have some



*An emotional display by Kenyatta University students following the death of a student.*

*Wanafunzi wenye hasira wa Chuo Kikuu cha Kenyatta, wakiandamana kulaani kifo cha mwenzao*

bearing on the licensing and operation of broadcasting stations and also of Internet websites. This would render the work of the PressTask Force, until now holding a mandate to make recommendations in such matters, irrelevant. It remains to be seen how the Kenyan Parliament will respond to the draft bill when it is tabled for discussion.

Clearly, radio and television are deeply significant for a community like East Africa as it strives to rebuild a once vibrant co-operation across its borders. In the absence of licences in Kenya, the Nation group is continuing vigorously to pursue opportunities in the more liberalised broadcasting markets of Tanzania and Uganda. Your Board remains confident that the group's efforts, in line with the world-wide trends to which I have referred, to enter the broadcasting markets of East Africa is the right strategy for the longer term, although it is clear that with relatively undeveloped advertising markets in both Tanzania and Uganda any major financial benefit has to be seen as a long term goal rather than a short term benefit.



*World famous photojournalist Mohamed Amin, a victim of the hijacked Ethiopian Airliner disaster*

*Mpiga picha maarufu ulimwenguni, Mohamed Amin, aliyefariki kwenye ndege iliyotekwa nyara ya Ethiopian Airlines*

**Dividend proposal and bonus issue**

Profit after taxation attributable to shareholders increased by 6% to Kshs. 206.9 million (Kshs. 195.1 million in 1995). An interim dividend of 12.5% (12.5%) was paid in October 1996 and taking account of the group's continued strong trading position and in view of the high dividend cover in recent years, the Board recommends a final dividend of 42.5% ( 32.5%). This brings the total for 1996 to 55% compared to 45% previously, an overall increase of 22%.

In addition to the increased dividend, your Board recommends for your approval a bonus issue of one fully paid-up share for every two shares held in the issued and paid-up share capital of the group. This bonus issue will be subject to the approval of the necessary authorities. Therefore these bonus shares will not qualify for the final dividend in respect of 1996.

The proposed increased final dividend and bonus issue reflect the directors' continuing confidence in the future of your company.

**Future prospects**

The severe drought conditions experienced at the start of the year have contributed to a significant reduction in the rate of growth of the economy. However, the strength in depth of all the group's publications has meant that despite the depressed economic background the group has made a promising start to 1997.

As mentioned earlier, the group is poised and ready for expansion into broadcasting throughout the region and is also actively pursuing a number of opportunities in the print media both within and outside Kenya.

In an election year, provided that the present stable exchange rate and subdued levels of inflation are maintained, your company expects to look forward to an excellent demand for its publications and as liberalisation continues we anticipate further positive developments in the year ahead.

**Directors and staff**

During the year the Group Finance Director Mr. Stuart Martin retired after six years valuable service with the company. His sound advice will be much missed by the Board and his colleagues. His successor, Mr. Richard Henry, joined the Board in December 1996. He brings valuable experience having previously worked in Kenya and having been Finance Director and Company Secretary of the Press Association in the United Kingdom for the last twelve years.

Finally, I would like to take this opportunity to thank our Managing Director, Mr. Wilfred Kiboro and our other executive directors as well as the managers and staff for their dedication and outstanding hard work, reflected in the excellent results achieved, in what was a demanding year. And, I should also like to pay tribute, to the members of the Board who as Chairmen or Members of specially created committees, such as the Finance and Audit Committee, the Editorial Committee and the Strategic Planning Committee, have devoted a great deal of time and provided valuable inputs at a time of considerable expansion and development for the group. In this environment, our executives and staff have responded to the challenges and opportunities with energy and enthusiasm. This dedication will enable us to continue to drive forward the company's future development.

B M Gecaga

**DR. B. M. GECAGA**
Chairman

**Matokeo ya kundi hili**

Mwaka jana ulikuwa mojawapo wenye ufanisi mkubwa kwa kundi hili lako. Uchumi wa Kenya ulibakia tumainifu katika kipindi cha kwanza cha mwaka huo. Hata hivyo, hii haikufanikishwa katika kipindi cha pili ambapo ufanisi wa kiuchumi uliteremka sana chini ya asilmia 5% iliyonakilishwa katika miezi sita ya kwanza.

Mwaka jana, niligusia kwenye ripoti yangu kuhusu ustawi kufuatia uamuzi wa Halmashauri wa kubadilisha mitambo iliyozeeka ya uchapishaji ya kundi hili. Kazi ya uwekaji wa mitambo mipya ya uchapishaji katika kiwanda chetu kilichoko Mombasa Road ilianzishwa mnamo Desemba 1995 na kukamilika katika muda wa miezi 12 na kuanza kutumika kwa uchapishaji. Kupitia kampuni ya Kijerumani, Koenig & Bauer-Albert AG, tuliweka mitambo ya kuweza kuchapisha nakili 60,000 za magazeti kwa saa.

Mpango huu kabambe sio tu kukamilika katika muda uliowekwa, lakini pia kulingana na bajeti ya Kshs. 750 milioni iliyokadiriwa mwanzoni. Sasa, tunajivunia mitambo mipya ya uchapishaji ambayo pia ndiyo ya kisasa zaidi kupatikana po pote katika Afrika. Rasilmali yetu, mojawapo wa kubwa zaidi kuwekwa na kampuni yo yote ya sekta ya kibinafsi nchini Kenya, inatuwezesha kuimarisha uchapishaji bora na hata utumizi wa picha za rangi kwa magazeti yetu yote.

Kuanzishwa rasmi kwa mitambo mipya ya uchapishaji ya Nation mnamo Machi, ilihudhuriwa na Mheshimiwa Rais wa Kenya, mwenye hisa zaidi Muadhama Aga Khan pamoja na wageni wengine mashuhuri. Kufaulu kwa sherehe hiyo kulikuwa thibitisho la juhudi kubwa na bidii ya wale wote waliohusika.

Mapato imara na matumizi ya pesa taslimu yaliyozingatiwa na kundi hili katika miaka ya hivi karibuni yalimaanisha kwamba zaidi ya nusu ya gharama ya mitambo hiyo mipya ya uchapishaji, zilipatikana humu na kiasi kilichobakia kupitia kwa mikopo ya muda wa kadiri ya banki. Licha ya ongezeko lililofuatia la malipo ya juu kwa riba ya mikopo, nina furaha kueleza kwamba kundi hili limepata tena matokeo mazuri katika hesabu zake.

Mapato kwa jumla ya kundi hili yaliimarika kwa asilimia 23% hadi Kshs. 1,895.7 milioni (kulinganishwa na Kshs. 1,538.0 milioni mnamo 1995). Kwa mara nyingine tena, Nation Newspapers Limited ndiyo ilikuwa ndio nguzo muhimu katika matokeo ya kundi hili ikiwa faida yake ya kibiashara ikiongezeka kwa asilimia 25%. Faida ya kibiashara ya kundi hili ya Kshs. 357.4 milioni (Kshs. 294.7 milioni) ilikuwa asilimia 21% zaidi ya mwaka 1995. Hata hivyo, faida ya kundi hili kabla ya kodi na matumizi maalumu ya Kshs. 262.1 milioni (Kshs. 296.9 milioni) ilikuwa Kshs. 34.8 milioni chini ya mwaka jana, kutokana na ongezeko la malipo ya juu kwa riba kutokana na rasilmali iliyowekwa katika mitambo mipya ya uchapishaji. Licha ya kuongezeka kwa gharama za faida kwa mkopo kiasi cha Kshs. 79 milioni, faida kwa wenye hisa, baada ya matumizi maalumu, ilikuwa Kshs. 206.6 milioni (Kshs. 195.1 milioni) na ambayo ilikuwa asilimia 6% juu ya mwaka uliotangulia.

**Nation Newspapers Limited**

Kampuni hii yenu muhimu ya magazeti ilipata tena matokeo mazuri na kuweka rekodi mnamo 1996. Bei za magazeti, *Daily Nation* na *Sunday Nation*, ziliongezwa kwa Kshs. 5 mnamo Machi 1996. Hii ilikuwa mara ya kwanza bei hizo kuongezwa kwa muda wa miaka miwili na zilikuwa chini ya kiwango cha gharama za maisha kwa kipindi hicho. Mauzo yao yaliteremka mwanzoni kufuatia ongezeko hilo la bei, ingawaje yalisawazika kamili kufikia mwishoni mwa mwaka. Magazeti yote mawili ya Kiswahili ya kampuni hii, *Taifa Leo* na *Taifa Jumapili*, pia yalishuhudia mafanikio ya maana katika ongezeko la uuzaji katika mwaka huo.

Wakati huo huo, gazeti la kila wiki la kampuni hii katika kanda hili, *The EastAfrican* lililoanzishwa mnamo 1994, lilishuhudia ongezeko imara katika uuzaji huku gazeti hilo likijikuza mathubuti kote nchini

CMA - LIBRARY



*Evander Holyfield, Mike Tyson fight in Las Vegas America*

*Pigano kati ya Evander Holyfield na Mike Tyson mjini Las Vegas, Amerika*

## Ripoti ya Mwenyekiti
**inaendelea**

Kenya, Uganda na Tanzania kama gazeti bora muhimu linalohitajika sana la habari za biashara katika Afrika Mashariki. *The EastAfrican* haikutimiza tu shabaha zake katika uuzaji zaidi na matangazo, lakini pia liliimarika katika kuleta faida katika mwaka huo. Hii ilikuwa mafanikio makubwa sana kwa gazeti lenye upeo mkubwa kama huo. *Gazeti hili linaendelea kusifika sana si tu kote katika kanda hili lakini pia kwingineko. Katika magazeti yetu yote, matangazo* yalibakia *imara kote* katika mwaka huo huku kukiwa na ufanisi bora wa kufana wa mapato na vipimo vya matangazo licha ya nyongeza kubwa sana za kiwango cha ada ya malipo ya matangazo mapema mwaka huo. Kutokana na hali hiyo, magazeti ya *Nation* na *Taifa* yalishuhudia tena nyongeza za maana katika mgawo wao wa mauzo. Matokeo hayo yanatokana na imani wa wasomaji na watangazi katika hali ya juu ya ubora ya magazeti ya Kiingereza na Kiswahili ya kampuni hii.

Mapato yaliyotokana na ongezeko *la* uuzaji na matangazo *katika magazeti haya ndiyo yalikuwa chanzo kikuu cha mapato yaliyoimarika ya kampuni hii ya Kshs.* 1,877.7 milioni, ongezeko la Kshs. 384.7 milioni (asilimia 26%) juu ya mwaka 1995.

Bei za makaratasi ya uchapishaji zilizoongezeka sana kuwa ghali mnamo 1995, na kudumika katika kipindi cha kwanza cha mwaka huo kabla kuteremka taratibu katika kipindi cha pili. Na kutokana na hali hiyo, kwa mwaka huo wote kwa jumla, ongezeko hilo lilihifadhika kwa, Kshs. 78.0 milioni (asilimia 16% juu ya 1995). Hata hivyo, gharama nyingine ziliongezeka kwa zaidi ya asilimia 30% kutokana na msimamo wa kampuni wa kusisitiza ubora wa magazeti yake na kudumisha viwango vya mishahara na malimbikizo kufikia makampuni ya kuifananisha nayo nchini Kenya.

Kiwango cha juu kwa jumla cha *ongezeko la gharama pia kilinakilisha viwango vya juu kihistoria vya gharama.* Hata hivyo huku gharama wakati huu ikiwa chini kuliko ilivyokuwa kwa muda mrefu sana, nyongeza zijazo katika gharama zinatazamiwa kuwa chini kwa wastani kuliko mnamo 1996 kutokana na usimamizi mkali wa matumizi na, kufikia sasa, nyongeza nafuu pekee katika bei za vifaa vya kiasili vya kazi.

Shabaha moja inayoendelea tena tangu mwaka uliopita imekuwa katika kutilia mkazo zaidi uimarishaji ubora. maongozi na maadili zimesaidia sana katika kuwapa wafanya kazi wetu warsha za habari zenye shabaha mahsusi kuhusiana na ubora, kiwango kilichoongezeka cha kupevuka.

Huku mitambo yetu mipya ya uchapishaji ikifanya kazi, *fursa imechukuliwa kuchunguza upya maendeleo* yaliyofikiwa *na kampuni katika maongozi ya picha za rangi.* Halmashauri imeamua kuzingatia mpango makini wa picha zilizoimarishwa za rangi na kuongeza utumiaji wao taratibu kote katika magazeti yetu, zikiambatana na uwekaji rasilimali wa vifaa vya uchapishaji katika miezi za siku za usoni. Baadhi ya picha zetu sasa zinachukuliwa kwa kutumia filamu za rangi, hatua nyingine kubwa ya maendeleo.

Katika mwaka huo pia, kulikuwa na mabadiliko katika kuanza kutumia mitambo ya kisasa kupanga kurasa za magazeti badala ya mtindo wa ukataji safu za habari na makala na kupachika kurasani kama ilivyokuwa zamani. Hii ilitokana na rasilmali mpya zilizowekwa katika idara za habari na matangazo ambapo wafanya kazi *wanajitayarishia wenyewe kurasa kupitia kwa mitambo ya kompyuta na kuchukua jukumu* la zamani la watayarishaji kurasa za magazeti kwa mikono kabla ya uchapishaji. Hii imetuwezesha kujipatia faida kamili kuambatana na bidhaa safi zaidi na ukamilishaji kazi mapema.

*The EastAfrican* iliingia mwaka wake wa pili ikifurahia taratibu ongezeko la uuzaji na matangazo na katika hali yake sasa imejikuza imara katika soko la magazeti katika kanda hili. Mauzo yake yaliendelea kuongezeka haraka hivi kwamba katika miezi mitatu ya mwisho ya 1996 yakaongezeka kwa karibu asilimia 70% kuanzia tangu mwanzoni mwa mwaka. Baadhi ya wasomaji shupavu wa *The EastAfrican* wanapatikana *miongoni mwa wafanya biashara na wataalamu katika nchi hizo tatu* ilhali baadhi ya matangazo ni ya kibiashara ambapo, ni thibitisho jingine la jinsi gazeti hili linavyothaminika sokoni kama chombo mathubuti cha kuwafikia wenye rasilmali, wafanya biashara, wataalamu na walio mamlakani kote katika Afrika Mashariki na kwingineko. Kama thibitisho zaidi la upanuzi, wagawaji zaidi wa gazeti hilo waliteuliwa majuzi mjini Harare nchini Zimbabwe na Johannesburg katika Afrika Kusini.

Katika miezi ya hivi karibuni kampuni imeanzisha maendeleo kadha ili kuithibitisha kuwapo kwetu katika ulimwengu wa mawasiliano ya kompyuta katika takwimu na habari kwa lengo la kuongoza katika mawasiliano hayo (*Internet*) katika Afrika, ambayo yanalingana kamili na lengo la kuwa kundi linaloongoza la vyombo vya habari katika Afrika Mashariki. Makala ya *Nation ya Internet* yamepanuliwa sasa kushirikisha soko la hisa la Nairobi pamoja na habari za biashara ya hisa za kigeni na hutegemewa mara kwa mara na nchi zilizotawanyika mbali kama vile Norway na Marekani.

**Nation Marketing and Publishing Limited**

Mwaka jana nilieleza kwamba, kutokana na matokeo mabaya ya Nation Marketing and Publishing Limited, shughuli zake zilikuwa zichunguzwe upya. Kutokana na uchunguzi huo Halmashauri yenu iliamua kusimamisha shughuli za kampuni hii katika sehemu nyingi. Hata hivyo, huku uchumi na utalii unapoimarika, kuna matumaini ya kuchapisha tena daftari zake nyingine na jarida. Kampuni hii, kwa hivyo, itachunguza uwezekano wa kufufua angalau bidhaa zake kupitia mikataba ya ushirikiano kwa lengo la kuimarisha zaidi faida zao katika siku za usoni.

**Nation Carriers Limited**

Mwishoni mwa 1996, mwaka wa pili ambapo Nation Carriers Limited ilikuwa ikisimamiwa moja kwa moja na kundi hili, Nation Printers and Publishers ilijipatia hisa liliyosalia ya kampuni hii ya asilimia $33^1/_3$ % kutoka kwa Akamba Public Road Services Limited, na kufanya Nation Carriers Limited kumilikiwa kwa asilimia 100% na kundi hili kama kampuni yake ndogo.

Katika mwaka huo, kampuni hiyo lilifanya vyema sana katika kutosheleza mahitaji ya magari ya kusafirisha magazeti kutokana na ongezeko la uuzaji wa magazeti na uchapishaji wa kurasa nyingi. Licha ya hali za kusikitisha na kuharibika kwa barabara katika kila sehemu nchini, magazeti kwa jumla yaliwasili mapema wakati yalipotarajiwa huku visa vya ajali na kuharibika magari vikipunguka kwa jumla. Hata hivyo, hii ilitimizwa kwa gharama kubwa za ukarabati na usimamizi wa magari huku baadhi ya magari ya kampuni hii yakitimika kwa chini ya miaka mitatu.

Tuna imani kwamba mielekeo hii ya kutia moyo ya kampuni hii ndogo katika miaka miwili iliyopita hautadumishwa tu lakini pia kuimarishwa zaidi. Halmashauri imeidhinisha mnamo 1997 mipango ya kuhamisha kampuni hii hadi karibu na kiwanda kipya cha uchapishaji cha Nation Newspapers katika Mombasa Road ili kuhakikisha uthabiti zaidi katika siku za usoni.

**Industrial Promotion Building Limited**

Kama ilivyoelezwa awali, wakati Industrial Promotion Building (IPB) ilipojipatia mali za Diamond Trust nchini Kenya mnamo 1994, hisa za Kundi la Nation katika IPB ziliteremka kutoka asilimia 20% iliyohifadhi tangu 1988 hadi asilimia 16.4% mwaka jana. Mwishoni mwa



*A Zairean family flees ethnic fighting in his strife-torn country*

*Mwananchi wa Zaire na jamaa yake wakikimbilia usalama kuepuka vita vilivyokuwa vikiendelea nchini mwao*

1996, IPB ilitangaza toleo maalumu la hisa pamoja na, kukamilika kwa rasilmali ya mitambo hiyo mipya ya uchapishaji, Nation Printers and Publishers ilitumia nafasi hiyo sio tu kujipatia hisa hizo, lakini pia kujipatia hisa zaidi muhimu zinazohitajika kuiongezea hisa zake hadi kufikia asilimia 20% na hivyo kuhifadhi IPB katika hadhi ya kampuni shirikishi.

IPB inamiliki jumba la kisasa la fahari la Nation Centre katikati ya jiji la Nairobi na IPS Building miongoni mwa mali nyinginezo za kibiashara. Kampuni hii ambayo majuzi imejinunulia ploti nyingine ya kustawisha katika sehemu muhimu sana katika Mombasa, imeshuhudia matokeo yake ya kibiashara yakiendelea kuimarika.

**Kenya Litho Limited**

Mwaka jana niliripoti kwamba mahitaji ya kifedha ya kuiimarisha tena Kenya Litho Limited yangeongeza gharama zaidi kwa mapato ya kampuni kwa miaka ijayo. Kutokana na

jambo hilo na mahitaji yale muhimu kutoka kwa Nation Newspapers Limited ya kiwanda chake kipya cha uchapishaji, Halmashauri yako iliamua kuuza asilimia 41.7% ya hisa zake ili iweze kuzingatia mapato yake kwa shughuli hizo za kampuni kuu. Nina furaha kuripoti kwamba kulikuwepo na ongezeko lisilo la kawaida baada ya matumizi ya Kshs. 48.0 milioni.

**Utangazaji**

Katika miaka iliyopita, ripoti ya Mwenyekiti imekuwa ikitaja juhudi zinazofanywa na kundi hili kuanzisha rasilmali zaidi katika shughuli za radio na televisheni kote katika kanda la Afrika Mashariki.

Wajibu mkubwa umetimizwa na wasimamizi wenu, hasa zaidi katika mwaka mmoja uliopita, kutambua na kutimiza lengo hilo. Ni jambo la kuvunja moyo tena kulazimika kueleza kwamba hadi sasa, hakuna mafanikio yo yote yameonekana katika kupata leseni nchini Kenya, ingawaje maombi yo yote yameonekana katika kupata leseni nchini Kenya, ingawaje maombi mapya ya leseni za radio na televisheni yamewasilishwa.

Sasa ni miaka sita tangu, kuambatana na maongozi ambayo Serikali ya kufungua huru masafa ya utangazaji, Kundi la Nation limeomba leseni hizo za utangazaji. Itakuwa vibaya kujidanganya kwamba Halmashauri yenu haikuvunjika moyo kwamba hadi sasa hatujapata majibu ya kufaa, hasa kundi hili linapoendelea kuthibitisha ustadi, kama shirika la habari, ambao tunaamini hauna kifani kutoka kwa washindani wo wote wetu kote katika kanda hili.

Kote ulimwenguni, mashirika ya habari kama vile yetu, yanaendelea kujiona kama yanajishugulisha na shughuli zilizopanuka za mawasiliano - na kwa hivyo, yamekuwa yakishiriki kwa dhati katika utangazaji wa kawaida na wa kupitia mitambo ya *satellite* pamoja na mawasiliano ya kisasa ya *internet*.

Katika hatamu hii, hatua ya hivi karibuni ambayo inatazamiwa kuwa na madhara zaidi kwa vyombo vya habari kwa jumla ni uchapishaji wa Mswada wa Kitaifa wa Mawasiliano *(National Communications Bill)* kwa lengo la kuimarisha Shirika la Posta na Simu la Kenya. Mswada huo umetayarishwa, kwa miongoni mwa shabaha nyingine, kuamua maongozi ya kufaa ya kufungua huru masafa ya utangazaji, unaelekea pia kuwa na uhusiano katika utoaji leseni na shughuli za vituo vya utangazaji na huduma za mawasiliano za *internet*. Hii inapasa kuzima jukumu la Kamati ya Uchunguzi wa Sheria za Uandishi wa Habari nchini, ambayo hadi sasa imekuwa na kibali cha kutoa mapendekezo katika maswala kama haya, kuwa bure. Bado inangojewa kuonekana jinsi Bunge la Kenya litakavyopokea mswada huo wakati utakapowasilishwa mbele yake kujadiliwa.

Kama ilivyo, ni wazi kwamba radio na televisheni ni muhimu sana kwa jamii kama vile ya Afrika Mashariki kwa sababu zitasaidia kujenga upya ushirikiano unaohitajika sana wa kuvuka mipakani. Bila kupata leseni nchini Kenya, Kundi la Nation linaendelea kuchunguza zaidi nafasi nyingine kama hizo katika masafa yaliyofunguliwa huru ya utangazaji nchini Tanzania na Uganda. Halmashauri yenu bado ina imani kwamba juhudi za kundi hili, kuambatana na mielekeo ya sasa ya ulimwengu ambayo tayari nimeeleza, za kuingia katika masafa ya utangazaji katika Afrika Masharika ni mbinu muhimu sana kwa manufaa ya baadaye, ingawaje ni wazi kwamba kutokana na masoko ya utangazaji ambayo hayajastawishwa nchini Tanzania na Uganda, faida yo yote kubwa ya kifedha ni lazima ionekane katika upeo wa muda mrefu badala ya faida ya muda mfupi.

**Pendekezo la Mgawo wa Faida na Toleo Maalumu la Hisa**

Faida kabla ya kodi iliyowekewa wenyehisa iliongezeka kwa asilimia 6% hadi Kshs. 206.9 milioni (kuliganishwa na Kshs. 195.1 milioni mnamo 1995). Mgawo wa muda wa faida wa asilimia 12.5% (12.5%) ulilipwa mnamo Oktoba 1996 na kwa kutilia maanani hali imara ya kibiashara ya kundi hili. Na kutokana na thamani ya juu ya hisa katika miaka ya hivi karibuni, Halmashauri hii inapendekeza malipo ya mwisho ya mgawo wa faida ya asilimia 42.5% (32.5%). Hii inafanya jumla ya mgawo wa faida kwa mwaka huo kuwa asilimia 55% ikilinganishwa na asilimia 45% mnamo 1996, ongezeko la jumla ya asilimia 22%.

Pamoja na mgawo wa faida ulioongezeka, halmashauri yenu inapendekeza ili mkubali toleo maalumu la hisa za bakshishi la hisa moja iliyolipiwa kamili kwa kila hisa mbili zinazohifadhiwa



*Rare treat for Street Children at State House, Nairobi, hosted by President Moi*

*Sherehe isiyo ya kawaida iliyoandaliwa Machokoraa katika Ikulu ya Nairobi na Rais Moi*

katika mtaji wa hisa za bakshishi na zilizolipiwa kamili za kundi hili. Toleo hili maalumu la hisa za bakshishi litategemea kibali cha maafisa wanaohusika. Hivyo, hisa hizi za bakshishi hazitahesabika katika mgawo wa mwisho wa faida kuambatana na 1996. Mgawo wa mwisho uliopendekezwa wa kuongezeka pamoja na toleo maalumu la hisa za bakshishi zinathibitisha imani inayoendelea ya wakurugenzi wenu katika hali ya baadaye ya kampuni yenu.

**Matumaini ya baadaye**

Ukame mbaya ulioshuhudiwa mwanzoni mwa mwaka huo ulichangia katika kupunguza sana kiwango cha ufanisi wa uchumi. Hata hivyo, kutokana na umaarifu na sifa za magazeti yote ya kundi hili, kuna maana kwamba licha ya msingi wa kiuchumi ulielezwa, kundi hili limeanza mwaka 1997 kwa matumaini.

Kama nilivyotaja awali, kundi hili limejiandaa barabara na lipo tayari kutekeleza mpango wake wa upanuzi katika rasilmali ya utangazaji kote katika kanda hili la Afrika Mashariki na linafuatilia kwa dhati nafasi nyingine kadha mpya katika uchapishaji nchini Kenya na nje.

Katika mwaka wa uchaguzi, mradi tu kiwango cha sasa thabiti cha ubadilishaji wa pesa za kigeni pamoja na viwango vya nafuu vya gharama za maisha zimedumishwa, kampuni yenu inatazamia kuona mahitaji yanayoongezeka ya magazeti yake na huku uchumi ukiendelea kufunguliwa huru zaidi, tunatumainia maendeleo zaidi ya manufaa katika mwaka unaoendelea.

**Wakurugenzi na wafanya kazi**

Katika mwaka huo, Mkurugenzi wa Fedha wa Kundi, Bw Stuart Martin, alistaafu baada ya utumishi wa kujivunia wa miaka sita na kampuni hii. Mawaidha yake ya busara yatakoswa sana na Halmashauri hii pamoja na wenzake. Mrithi wake, Bw Richard Henry, alijiunga na Halmashauri hii mnamo Desemba 1996. Analeta maarifa ya kuthamanika akiwa amewahi awali kufanya kazi nchini Kenya na kuwahi pia kuwa Mkurugenzi wa Fedha na Katibu wa Press Association nchini Uingereza kwa kipindi cha miaka 12 iliyopita.

Mwisho, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mkurugenzi Mkuu wetu, Bw Wilfred Kiboro, pamoja na wakurungenzi wetu wengine kwa kujitolea kazini kwa bidii na dhati, kama ilivyodhihirika katika matokeo bora ya kufana yaliyopatikana, katika mwaka ambao mara nyingi ulikuwa na shughuli nyingi. Na, ninapenda pia kuwapongeza, wanachama wa Halmashauri, ambao kama Wenyeviti ama Wanachama wa kamati zilizoundwa maalumu, kama vile Kamati ya Ukaguzi wa Fedha, Kamati ya Uhariri na Kamati ya Uratibu wa Mipango, wametumia muda wao mwingi sana na kutoa miongozo ya kuthaminika sana wakati wa upanuzi mkubwa na maendeleo ya kundi. Katika mazingira haya, warasimu wetu na wafanya kazi wamejitolea kwa juhudi na motisha kutekeleza kikamilifu wajibu wao. Imani hii imetuwezesha kuendelea kuimarisha zaidi maendeleo yajayo ya kampuni hii.



**DR. B. M. GECAGA**
Mwenyekiti

# Board of Directors

# Halmashauri ya Wakurugenzi



*Dr. B. M. Gecaga, C.B.S.*



*W. D. Kiboro*



*H. H. O. Awori*



*A. Bekah*



*R. C. Henry*



*L. Huebner*



*F. O. Okello*



*A. Poonawala*



*W. Robinson*



*J. D. M. Silvester*



*G. M. Wilkinson*

## Board of Directors

## Halmashauri ya Wakurugenzi

| | | |
|---|---|---|
| Chairman (Kenyan) | **Dr. B. M. Gecaga, C.B.S.** | *Mwenyekiti (Mkenya)* |
| Chief executive / managing (Kenyan) | **W. D. Kiboro** | *Mrasimu mkuu/Msimamizi (Mkenya)* |
| (Kenyan) | **H. H. O. Awori** | *(Mkenya)* |
| (Kenyan) | **A. Bekah** | *(Mkenya)* |
| (British) | **R. C. Henry** | *(Mwingereza)* |
| (American) | **L. Huebner** | *(Mmarekani)* |
| (Kenyan) | **F. O. Okello** | *(Mkenya)* |
| (French) | **A. Poonawala** | *(Mfaransa)* |
| (Australian) | **W. Robinson** | *(Mwa—Australia)* |
| (Kenyan) | **J. D. M. Silvester** | *(Mkenya)* |
| (Irish) | **G. M. Wilkinson** | *(Mwa—Irish)* |

| | | |
|---|---|---|
| Secretary | **S. G. Ogutha, CPA(K), CPS(K)** | *Katibu* |
| Registered office | **Nation Centre<br>Kimathi Street<br>Nairobi** | *Afisi Ilikoandikishwa* |
| Auditors | **Coopers & Lybrand<br>Queensway House<br>Kaunda Street<br>Nairobi** | *Wakaguzi wa Hesabu* |
| Bankers | **Standard Chartered Bank Kenya Limited<br>Stanbank House<br>Moi Avenue<br>Nairobi** | *Banki* |
| Solicitors | **Hamilton, Harrison & Mathews<br>ICEA Building<br>Kenyatta Avenue<br>Nairobi** | *Wakili* |
| Subsidiary companies | **Nation Newspapers Limited<br>Nation Marketing & Publishing Limited<br>Nation Carriers Limited** | *Makampuni Madogo* |
| Associated company | **Industrial Promotion Building Limited** | *Kampuni iliyoshirikishwa* |

CMA-LIBRARY

# Directors' Report

The directors have pleasure in presenting their report and the audited accounts for the year ended 31st December, 1996.

**Group results**
The results of the group for the year are as set out in full in the profit and loss account on page 20.

**Dividends**
The directors recommend the payment of a final dividend of 42.5 % on the issued share capital at 31st December, 1996, which, together with the interim dividend of 12.5% paid on the 30th October, 1996, makes a total of 55% in respect of the year ended 31st December, 1996.

**Directors**
The present Board of directors is as set out on page 3. Mr. R. C. Henry was appointed to the Board on December 5, 1996. All the other directors have been directors throughout the year. Mr. R. C. Henry, retires in accordance with Article 96 while Mr. H. H. O. Awori, Mr. A. Poonawala and Mr. W. Robinson retire by rotation in accordance with Article 110. Being eligible, they offer themselves for re-election.

**Auditors**
Coopers & Lybrand will continue in office in accordance with Section 159(2) of the Companies Act (Cap 486).

Approved by the Board,
S.G. Ogutha
Secretary

10th April, 1997



# Taarifa ya Wakurugenzi

Wakurugenzi wana furaha kutoa ripoti yao pamoja na hesabu zilizokaguliwa kuhusu mwaka uliomalizika Desemba 31, 1996.

**Matokeo ya kundi:**
Matokeo ya kundi kuhusu mwaka huo ni kama yalivyoonyeshwa kikamilifu katika taarifa ya hesabu ya faida na hasara kwenye ukurasa wa 21.

**Migawo ya faida:**
Wakurugenzi wanapendekeza malipo ya mwisho ya mgawo wa asilimia 42.5 kuhusu hisa zilizotolewa za mtaji kufikia Desemba 31, 1996, ambao, pamoja na mgawo wa muda wa faida wa asilimia 12.5% uliolipwa Oktoba 30, 1996, unajumlisha mgawo kuhusu mwaka uliomalizika Desemba 31, 1996 kuwa asilimia 55.

**Wakurugenzi:**
Halmashauri ya sasa ya Wakurugenzi ni kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 3. Bw. R.C. Henry aliteuliwa katika Halmashauri ya Wakurugenzi mnamo Desemba 5, 1996. Wakurugenzi wengine wote walioelezwa hapo walikuwapo mwaka wote.

Bw. R.C. Henry anastaafu kulingana na kifungu cha 96 ilhali Bw H. H. Awori, Bw A. Poonawala na Bw. W. Robinson wanastaafu kwa zamu kulingana na kifungu cha 110. Wote, kwa sababu wanaweza kuchaguliwa, wamejitolea tena kuchaguliwa wakurugenzi.

**Wakaguzi wa hesabu:**
Kampuni ya Coopers and Lybrand itaendelea kukagua hesabu za kundi kulingana na kifungu cha 159(2) cha Sheria ya Kampuni (Ukurasa wa 486).

